SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la

# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 24, Oktoba 2022

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# KAMATI ZA BUNGE ZASAFIRI KWA SGR DODOMA HADI DAR ES SALAAM



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC, Masanja Kungu Kadogosa akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi wa SGR kwa wenyeviti wa kamati ya bunge, ndani ya treni ya mhandisi wakati walipotembelea kuona maendeleo ya mradi wa SGR Dodoma - Dar es salaam, Septemba 2022.

**Na Mwandhishi wetu**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Kamati ya Uwekezaji Mitaji ya Umma zimefanya ziara ya kutembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR unaotekelezwa na Shirika la Reli Tanzania - TRC kuanzia Dodoma hadi Dar es Salaam kwa kutumia treni ya uhandisi ya SGR Septemba 26, 2022.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Mhe. Selemani Kakoso amesema "leo tumefanya ziara kutembelea mradi wa SGR unaotekelezwa na TRC na kujionea namna mradi huo unavyotekelezwa",

Mhe. Kakoso ametoa wito kwa Shirika la Reli na kuwataka washirikiane na Serikali kuhakikisha reli inafika katika nchi za jumuiya ya Afrika mashariki.

Inaendelea Uk. 2

## TRC YAZINDUA MAFUNZO KWA WATENDAJI WATAKAOSIMAMIA UENDESHAJI WA SGR

**Uk. 3.**




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Masanja Kungu Kadogosa akifungua mafunzo kwa vitendo ya matayarisho kwaajili ya uendeshaji wa reli ya kisasa - SGR katika ukumbi wa TRC jijini Dar es salaam Septemba, 2022

# KAMATI ZA BUNGE ZASAFIRI KWA SGR DODOMA HADI DAR ES SALAAM

Inatoka Uk. 1

"Tunawaomba TRC kufanya jitihada kwa kushirikiana na Serikali kuhakikisha kipande cha kutoka Tabora - Kigoma kinakamilika haraka. Lakini tunaiomba Serikali wafanye jitihada ya kuunganisha nchi jirani hasa Kongo ambako kuna mizigo mingi na yenye tija katika bandari zetu kwa kufanya hivyo tutaona faida kubwa ya uwekezaji katika reli yetu" alisema Mhe. Kakoso.

Vilevile Mhe. Kakoso amebainisha kuwa endapo mradi wa SGR utavuka mipaka kwenda nchi jirani kama Kongo, Sudani kusini na Burundi bandari za Dar es Salaam, Mwanza na Tanga zitanufaika na kuongeza uchumi wa nchi na kuchochea maendeleo kwa watanzania.

"Tunaamini endapo Serikali itawekeza katika kupeleka SGR kwenye nchi jirani tutapanda kutoka asilimia 37% za mizigo tunazopata kutoka bandari ya Dar es Salaam, tuna uwezo wa kufika 60% mpaka 70% kwasababu tutakua na eneo kubwa la upitishaji mizigo kutoka Kongo kupitia Zambia kupitia bandari ya Kalemi kuja bandari Karema na kuunganisha reli ya kutoka Mpanda hadi Dar es Salaam." aliongeza Mhe. Kakoso.

Pia, Mhe. Kakoso ameieleza TRC kuwa, kutakuwa na mzigo mwingine mkubwa kutoka Uganda kupitia bandari ya Dar es Salaam na Tanga ambapo kutakuwa na kiwango kikubwa cha ubebaji mizigo kutoka 2% ya mzigo inayopitia bandari ya Dar es Salaam na kufikia 30%, hivyo mizigo ya Uganda ikipitia bandari ya Dar es Salaam itateka soko la Sudani Kusini.

Kwa upande wake George Malima, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji Mitaji ya Umma amesema lengo la ziara ni kuona kazi inayofanyika na kwenda kuwaambia wananchi kile ambacho wamekiona.

"Tumeona kwa macho yetu uwekezaji mkubwa uliofanyika na unaoendelea tunaipongeza TRC kwa usimamizi mzuri. Sisi kama wawakilishi wa wananchi tunakuwa katika nafasi nzuri ya kuwaambia wananchi uhalisia wa mradi" alisema Mhe. Malima.

Mhe.Malima aliongeza kuwa "mradi huu umejengwa katika ustadi mkubwa sana na tunaiona fedha iliyotumika, niwaombe TRC na watanzania kwa ujumla kuwa walinzi wa miundombinu hii, kwa kufanya hivyo tutakuwa na fursa ya kuwavutia wawekezaji wengi kuja kuwekeza nchini".

Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa akijibu swali la Mhe. Kakoso, ameelezea ni kwa namna gani Shirika limejipanga kulinda miundombinu dhidi ya uhujuma.

"Tunashirikiana na vyombo vyote vya ulinzi na usalama kuhakikisha miundombinu hii inabaki salama, katika stesheni zote tumejenga vituo vya polisi ili kuhakikisha usalama wa miundombinu na abiria sambamba na hivyo Shirika linaendelea kutoa elimu ya uelewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa wananchi kuhusika katika ulinzi wa miundombinu ya reli" alisema Mkurugenzi Mkuu TRC.

Wajumbe waliridhishwa na maendeleo ya mradi kwani wamepata fursa ya kusafiri kwa reli ya SGR kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam umbali wa Km 444. Wajumbe ambao ni wawakilishi wa wananchi Bungeni wameieleza TRC kuwa wataendelea kuwa mabalozi wazuri katika kuutangaza mradi na kuusemea kwa wananchi.



Mkurugenzi Mkuu TRC, Masanja Kungu Kadogosa (kulia) akitoa maelezo ya uendeshaji treni kwa wajumbe katika chumba cha kuongozea treni katika stesheni ya Morogoro wakati walipotembelea kuona maendeleo ya mradi wa SGR Dodoma - Dar es Salaam, Septemba 2022.

# TRC YAZINDUA MAFUNZO KWA WATENDAJI WATAKAOSIMAMIA UENDESHAJI WA SGR

Shirika la reli Tanzania - TRC limezindua mafunzo kwa vitendo kwa watendaji wa TRC yatakayotolewa na wataalamu kumi na watano (15) kutoka Shirika la Reli la Korea – KORAIL, katika ukumbi wa mikutano makao makuu TRC jijini Dar es Salaam Septemba 28, 2022.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa amesema mafunzo haya ni utekelezaji wa mkataba wa mafunzo kwa vitendo uliosainiwa tarehe 4 Julai 2022 mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassani Ikulu Jijini Dar es Salaaam kati ya TRC na KORAIL.

“Haya ni maandalizi ya uendeshaji wa treni ya kisasa ambayo miundombinu yake kwa kipande cha kwanza cha Dar es Salaam hadi Morogoro imekamilika kwa zaidi ya asilimia 97 na kipande cha pili kutoka Morogoro hadi Makutopora kimekamilika kwa zaidi ya asilima 91” amesema Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Kadogosa.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Kadogosa amesema Shirika limeamua kuwatumia KORAIL kutoa mafunzo kwa vitendo kwa watendaji wa TRC kwasababu uendeshaji wa treni ya kisasa Korea ya Kusini ni salama kwa asilimia 99.9, hii inaonesha wana wataalamu waliobobea katika nyanja zote za uendeshaji wa treni ya kisasa.

Baadhi ya nyanja ambazo wataalamu wa KORAIL watatoa mafunzo ya nadharia na vitendo ni jinsi ya kupanga treni, uongozaji wa treni, uendeshaji wa treni, biashara ya treni, kutoa utaalamu wa karakana ziweje na usafirishaji katika uendeshaji wa treni. Mafunzo yatakuwa ni ya kina nayatatolewa kwa muda wa miaka mitatu.

“Ili kupata elimu nje ya muda wa kazi ni vyema kuwa na uhusiano mzuri na wataalamu hawa kutoka KORAIL kwa sababu watakuwa TRC kwa muda mrefu” amesisitiza Ndugu Kadogosa.

Mkurugenzi Mkuu TRC ametoa ufafanuzi kuwa uendeshaji wa treni ya kisasa utaanza rasmi mwezi Februari 2023 baada ya taratibu zote za majaribio kufanyika na kukubaliana gharama za usafirishaji na Mamlaka ya Udhibiti Usafi Ardhini - LATRA.

Naye Meneja wa mradi kutoka KORAIL Ndugu Lee Seung Young ameshukuru uongozi wa TRC kwa kuwaamini kwa kazi ya utaoaji mafunzo kwa vitendo katika uendeshaji wa treni ya kisasa na kuahidi kutoa mafunzo kwa ufanisi kwasababu wamekuja na wataalamu katika nyanja mbalimbali na wana uzoefu wa kutosha kwenye uendeshaji wa treni ya kisasa.

Mafunzo kwa vitendo kwa uendeshaji wa treni ya kisasa yatashirikisha watendaji vijana zaidi ya thelathini kutoka TRC na wataalamu kumi na tano kutoka KORAIL.



Picha ya pamoja ni Mkurugenzi Mkuu wa TRC, baadhi menejimenti ya TRC na wawakilishi wa Shirika la reli korea wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa vitendo ya matayarisho kwaajili ya uendeshaji wa reli ya kisasa - SGR katika ukumbi wa TRC jijini Dar es salaam, Septemba, 2022

# TRC, TANAPA KUSHIRIKIANA KUKUZA UTALII WA NDANI

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC washirikiana na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania - TANAPA kukuza utalii wa ndani baada ya kutembelea stesheni ya Mvave iliyopo karibu na mbuga ya Saadani mkoa wa pwani hivi karibuni Septemba, 2022.

Stesheni ya Mvave ambayo iko mbioni kufungiliwa mara baada ya kukamilika kufanyiwa ukarabati na italeta hamasa kwa wananchi pamoja na wageni wanaotumia usafiri wa reli kwenda kutalii katika mbuga ya Saadani.

Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara TRC Bw. Never Diamond ameeleza kuwa ushirikiano baina ya TRC na TANAPA ni kuangalia miundombinu wezeshi ya kibiashara kati yao kujua jinsi ya kukuza utalii wa ndani kupitia usafiri wa treni.

“Treni ni usafiri mwepesi sana kwa abiria unaotumia gharama nafuu pia treni ni zaidi ya safari“ alisema Bw. Diamond.

Pia Bw. Diamond alisema kuwa stesheni ya Mvave ni stesheni muhimu katika kukuza utalii hivyo TRC na TANAPA imeweka mikakati mbalimbali ambayo itawezesha wananchi watumie muda wao kwenda kupumzika na kuona vivutio vilivyopo nchini.

“TRC tunaunga juhudi za Raisi wetu Samia Suluhu Hassan katika kukuza utalii wa ndani (Royal Tour)” alisema Bw. Diamond.

Naye Kamishina Msaidizi wa Uhifadhi, kutoka katika Hifadhi ya Taifa Saadani Bw. Ephraim Mbomo amesema kuwa kituo cha Mvave kitabadilisha uwezo wa kupokea wageni wanaotumia magari ya kukodisha na kupata huduma ya moja kwa moja kwa kutumia usafiri wa treni. Treni ni usafiri wa uhakika katika vipindi vyote masika na kiangazi sababu wakati wa masika magari hupata shida kutokana na miundombinu ya barabara“ alisema Bw. Mbomo.

Aidha, Bw. Mbomo alieleza kuwa kwa mwaka hupokea wageni kwa wastani wa elfu 20 hivyo kupitia usafiri wa treni idadi ya wageni itaongezeka.

“Tumejipanga kuwapokea wageni watakaoongezeka, tayari tuna eneo la 'dining' lenye uwezo wa kuhudumia watu 300 pamoja na eneo la kambi ili tuweke mahema ya kutosha” alisema Bw. Mbomo.

Vilevile Bw. Mbomo alitoa shukrani kwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kupitia uzinduzi wa Royal Tour ambapo umeleta ongezeko kubwa la watalii kuja kuona vivutio mbalimbali nchini.

“Hifadhi ya Saadani ni hifadhi pekee ambayo mbuga imekutana na bahari“ alisema Bw. Mbomo.

Pia Afisa Utalii Bw. Athmani Mbae alisema kuwa hifadhi ya taifa ya Saadani ina jumla ya kilometa 1,100 ambayo ina vivutio mbalimbali vya wanyama wakiwemo Faru, Simba, Tembo, Twiga, Chui, Nyati , Mamba, Viboko , Swala na pia kuna aina za ndege wa nchi kavu, baharini pamoja na mto Wami.

“Kivutio hiki kina makutano ya mto Wami unaotoka Dodoma na kukutana na bahari ya hindi” alisema Bw. Mbae.

Huduma za utalii zinazopatikana katika hifadhi hiyo ni pamoja na utalii wa boti ili kuweza kuona viboko na mamba kiurahisi, utalii wa kutumia magari pamoja na kutembea kwa miguu pamoja na utalii wa usiku kutokana na wanyama ambao sio rahisi kuonekana mchana pamoja na michezo mbalimbali.

# BENKI YA TCB YARIDHISHWA MAENDELEO YA MRADI WA SGR



Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Umeme Mhandisi Tito Mateshi kutoka TRC (kulia) akielezea kuhusu miundombinu ya reli iliyopo katika stesheni ya Ruvu katika ziara iliyofanywa na menejimenti kutoka benki ya TCB hivi karibuni Agosti, 2022.



Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Umeme kutoka TRC Mhandisi Tito Mateshi (kulia) akionyesha ramani ya jengo la stesheni kuu ya SGR iliyopo jijini Dodoma kwenye ziara iliyofanywa na benki ya TCB hivi karibuni Agosti, 2022.

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limepokea ugeni wa menejimenti kutoka benki ya TCB na kutembelea mradi wa Reli ya Kisasa – SGR kipande cha kwanza Dar es Salam – Morogoro katika jengo la Stesheni ya reli ya kisasa lililopo jijini Dar es salaam hivi karibuni Agosti, 2022.

Ziara ya menejimenti ya benki ya TCB imelenga kujionea maendeleo ya mradi wa ujenzi wa SGR ili kudumisha uhusiano uliopo baina ya benki ya TCB na TRC.

Mkurugenzi Mkuu TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa amesema kuwa TCB imekua ikitoa fedha kwa TRC ili kuhakikisha miundombinu ya reli inaendelea kuwa maradufu hivyo benki hiyo imekua mdau mkubwa katika kuleta maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya reli nchini.

"TCB ni benki ya serikali na ni mdau muhimu sana sio tu kwa SGR, TCB ndio benki pekee iliyotuamini na kutupatia zaidi ya Bilioni 12 kipindi cha TRL, tunawashukuru sana" alisema Ndugu Kadogosa.

Pia Kadogosa alieleza kuwa kupitia mradi huo wa SGR benki zitapata fursa ya kuweka mashine za kutolea fedha (ATM) pamoja na ofisi katika stesheni zilizopo kuanzia Dar es Salaam hadi Mwanza hivyo ni vyema kuendelea kudumisha mahusiano baina ya TRC na mabenki.

"Tunakoenda tutahitaji maofisi zikiwemo benki pamoja na ATM ambazo wananchi wataweza kufanya miamala ya kuweka na kutoa fedha katika stesheni zetu za SGR" alisema Kadogosa.

Hata hivyo Mkurugenzi Mkuu ameeleza kuwa mradi huo wa SGR una wakandarasi kwa awamu ya kwanza ambayo ina vipande vitano kuanzia Dar es Salaam hadi Mwanza hivyo fedha zilizotumika kutoka kwenye benki hiyo zimezaa matunda katika kuendeleza mradi wa SGR.

Naye Mwenyekiti wa Bodi kutoka benki ya TCB Dkt. Edmund Mndolwa alisema kuwa hatua iliyofanyika katika ujenzi wa mradi huo wa kimkakati ni kubwa kuanzia ujenzi wa stesheni hadi miundombinu ya reli pamoja na mifumo mbalimbali ya uendeshaji wa treni hiyo ya kisasa.

"Wananchi sasa wataweza kufanya kazi Dodoma na Kulala Dar es Salaam bila kupoteza muda safarini" alisema Dkt. Mndolwa.

# WAKUFUNZI KUTOKA KORAIL WAFANYA ZIARA KATIKA MRADI WA SGR DAR - MORO



Wakufunzi kutoka kampuni ya KORAIL na baadhi ya watumishi wa TRC wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kufanya ziara katika mradi wa SGR Septemba, 2022.

**Na Mwandishi wetu**

Wafanyakazi zaidi ya 30 wa Shirika la Reli Tanzania - TRC wakiambatana na wataalamu 15 kutoka Shrika la Reli la Korea - KORAIL wamefanya ziara ya siku mbili kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro Septemba 2022.

Lengo la ziara ni kujionea vituo vya reli ya kisasa na miundombinu kwa kipande cha kwanza Dar es Salaam - Morogoro ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mkataba wa mafunzo kwa vitendo uliosainiwa Julai 4 2022 mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan Ikulu jijini Dar es Salaam kati ya TRC na Shirika la Reli la Korea.

Aidha Mratibu wa Mradi wa SGR Mhandisi Faustine Kataraia ameelezea kuwa njia zitakazotumika katika mafunzo ni pamoja na njia ya darasani na vitendo yatakayotolewa ndani ya nchi na nje ya nchi. Washiriki wa mafunzo hayo ni wafanyakazi wa TRC vijana zaidi ya 30.

Naye Meneja wa Mradi kutoka Shirika la Reli la Korea Mhandisi Lee Seung Yong amesema ziara hii ni mwanzo wa mafunzo kwa vitendo kwa kujionea vituo na miundombinu ya treni ya kisasa ili waweze kutoa utaalamu wa uendeshaji wa reli ya kisasa.

Kwa upande wa watendaji wa TRC ambao watapatiwa mafunzo kwa vitendo kuhusu uendeshaji wa treni ya kisasa wamesema wapo tayari kupokea mafunzo kutoka kwa wataalamu wa Shirika la reli la Korea na wao kuwa waalimu kwa watendaji wenzao.

Ziara imehitimishwa mkoani Morogoro ambapo wataalamu kutoka Shirika la reli Korea kila mtaalamu atakuwa na watendaji wawili kutoka TRC ili kuhakiksha wanawapatia utaalamu walionao kuhusu uendeshaji wa treni ya kisasa

# WATAALAMU MAMLAKA ZA HALI YA HEWA BARANI AFRIKA NA ULAYA WAZURU SGR



Baadhi ya wajumbe wa Mamlaka za Hali ya Hewa Barani Afrika na Shirika la "Satellite" Ulaya wakitazama miundo mbinu ya ujenzi wa reli ya kisasa - SGR katika stesheni ya Pugu walipotembelea mradi huo Septemba, 2022

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limepokea wajumbe takribani 150 kutoka Mamlaka za Hali ya Hewa Barani Afrika na Mashirika ya Satelite Barani Ulaya kutembelea ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Septemba, 2022.

Wajumbe kutoka nchi zaidi ya 70 kote duniani wakiambatana na mwenyeji wao kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) wamefanya ziara ya kutembelea ujenzi wa mradi wa SGR kipande cha Kwanza kutoka stesheni ya Dar es Salaam mpaka stesheni ya Pugu na kujionea maendeleo ya na ujenzi wa mradi huo.

Bwana Wilbert Timiza Mubuke Meneja wa Mahusiano ya Hali ya Hewa Kimataifa kutoka Mamlaka ya Hewa nchini ambaye pia ni mkuu wa msafara katika ziara hiyo amesema kuwa lengo la ziara hiyo ni kujionea jinsi gani sekta ya ujenzi wa miundombinu ya miradi mikubwa ukiwemo SGR na sekta ya usafirishaji wa nchi kavu unavyotegemea Mamlaka za Hali ya hewa katika shughuli zake.

"Mojawapo ya sekta inayotumia sana huduma hizo ni sekta ya usafiri wa nchini kavu hasa usafiri wa reli kwahiyo ndio maana tumekuja kuona mradi huu wa SGR kwa namna ambavyo unatumia hali ya hewa" amesema Bwana William Mubuke.

Aidha, Bwana Mubuke ameongeza kuwa baada ya kongamano hilo la 15 la Mamlaka za Hali ya hewa barani Afrika na Shirika la Setelite Barani Ulaya itarushwa 'Satellite' ambayo itakuwa na uwezo wa kutoa taarifa sahihi za hali ya hewa kwa uhakika na hivyo kuisaidia sekta ya usafirishaji wa reli kuendelea zaidi.

Miongoni mwa wajumbe hao katika ziara hiyo Meneja Mratibu Kongamano la Wataalamu wa Mamlaka za Hewa Afrika Bi. Mariane Diop Kane kutoka nchini Senegal ambaye ni ameeleza kufurahishwa kwake na ujenzi wa SGR ambao utaenda kuunganisha nchi nyingi za Afrika kijamii na kibiashara na kuleta maendeleo ya kiuchumi.

"Kwanza nimeoneshwa ofisi ya uhamiaji katika stesheni ya Dar es Salaam nikajiuliza ni ya nini, mwisho nikapata kufahamu kumbe SGR ni mradi wa Kimataifa, nimefurahishwa sana na ujenzi huu" Amesema Bi Mariane Diop.

Wajumbe wengi katika ziara hii wameeleza kufurahishwa kwao na ujenzi huu mkubwa wa mradi wa SGR na wameziomba nchi za Afrika kufanya uwekezaji wa namna hii katika kuleta maendeleo chanya Afrika.

## WANANCHI MKOANI SHINYANGA NA MWANZA WAPOKEA HUNDI ZA MALIPO YA FIDIA

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limeendelea na zoezi la kukabidhi hundi za malipo ya fidia kwa wananchi waliotwaliwa maeneo yao mkoani Shinyanga na Mwanza, Septemba 2022.

Hundi za malipo ya fidia zaidi ya 200 zimekabidhiwa kwa wananchi mkoani Shinyanga na Mwanza katika vijiji vya Isabilo, Mhulya, Mantare, Ligembe, Bujingu, Sokoni, Ihapa, Mwamalili, Nkalalo, Kang'anga, Ishingisha, Isunga, ili kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha Mwanza - Isaka.

Maeneo yaliyotwaliwa ni pamoja na, maeneo ya njia kuu kwaajili ya kupitisha njia ya reli na maeneo ya kuchukulia udongo unaotumika katika ujenzi wa reli ya kisasa.

Wananchi wa vijiji hivyo wameishukuru Serikali kwa kuwapatia malipo ya fidia ili waweze kufanya shughuli za maendeleo ikiwemo kilimo, ufugaji pamoja uendelezaji wa makazi kwa kujenga nyumba bora za kuishi.

Mwananchi wa kijiji cha Ihapa mkoani Shinyanga Bwana John Bundara Ndaka amesema kuwa zoezi la malipo ya fidia limekwenda vizuri na ameishukuru Serikali kwa kuwapatia stahiki zao ili waweze kuendelea na shuhuli za kimaendeleo kwani kiasi cha fedha walichopata kupitia fidia hizo kitawawezesha kujenga nyumba za kisasa na kununua ng'ombe na mashamba.

Zoezi limeendeshwa kwa usimamizi wa maafisa kutoka Shirika la Reli Tanzania, maafisa ardhi kutoka wilaya husika, viongozi wa vitongoji na vijiji kwa kushirikiana na maafisa wa benki ili kuhakikisha wananchi wanapata urahisi wa huduma za kibenki ikiwemo kufungua akaunti na kukabidhi hundi kwa usalama zaidi.




Mhandisi Bruno Kilowoko (kushoto) kutoka TRC akitoa elimu kuhusu taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi wa kijiji cha Ihapa mkoani Shinyanga kabla ya kuanza zoezi la ugawaji hundi za malipo ya fidia, Shinyanga, Septemba 2022.

# MATUKIO TOFAUTI KATIKA PICHA




Uongozi kutoka TRC pamoja na Uongozi kutoka Hifadhi ya Taifa ya Saadani wakiwa kwenye picha ya pamoja katika kituo cha stesheni ya Mvave iliyopo pembezoni mwa mbuga ya Saadani mkoani Pwani Septemba, 2022.



Timu kutoka TRC ikiongozwa na timu kutoka katika hifadhi ya taifa ya Saadani kufanya utalii wa ndani katika mto Wami uliopo ndani ya hifadhi ya taifa ya Saadani mkoa wa Pwani, Septemba 2022.



Muonekano wa jengo la stesheni ya reli ya kisasa jijini Dodoma



Mkufunzi kutoka KORAIL akiwapatia maelezo baadhi ya watumishi wa TRC kabla ya kuanza ziara katika mradi wa SGR Septemba 2022.



Treni ya uhandisi ikiwa inatoka ndani ya handaki la reli ya kisasa Kilosa mkoani Morogoro wakati wa ziara ya wajumbe wa kamati za bunge, Septemba 2022

# TRC YAENDELEA NA ZOEZI LA UTWAAJI ARDHI MKOANI SHINYANGA



Mkuu wa Idara ya ardhi na maliasili Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Bwana Julius Maira akizungumza na wakazi wa kijiji cha Puni wakati wa uelemishaji wa uhamishaji makaburi kupisha mradi wa SGR, mkoani Shinyanga Septemba 2022.

**Na Mwandishi wetu**

TRC imefanya zoezi la uhamishaji makaburi katika vijiji vya Didia, Sumbigu, Isholola, Puni, Nyashimbi, Zobogo, Bunonga na Sumbigu Wilaya ya Shinyanga vijijini Septemba 2022.

Zoezi hilo lina lengo la kutwaa maeneo kwaajili ya kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ikiwemo eneo la kumwaga kifusi pamoja na kuchimba kifusi katika kipande cha tano Isaka - Mwanza.

Mhandisi kutoka TRC Oliver Julius amewashukuru wananchi pamoja na viongozi wa vijiji kwa kutoa ushirikiano mzuri wa zoezi hilo la kuhamisha miili ya wapendwa wao kwenye vijiji hivyo.

"Tumetoa elimu ya uhamishaji makaburi katika vijiji vya Didia, Bunonga, Zobogo, Mwamanyuda, Isholola, Puni, Nyashimbi, Sumbingu na Bunonga" alisema Mhandisi Julius.

Afisa Afya wa Kata ya Didia Wilaya ya Shinyanga vijijini Bi. Eduardina Maganga amesema watu wa Afya wanahakikisha usalama wa wachimbaji, wazikaji pamoja na wafanyakazi wote wanaohusika na zoezi la uhamishaji wa makaburi kwa kuwapa vitendea kazi ikiwemo mipira ya kuvaa mikononi, barakoa na Dawa za kuwalinda dhidi ya magonjwa yaambukizayo.

"TRC imefanya jambo zuri kuweza kutushirikisha watu wa Afya kwenye hili zoezi kwani tunaweza kuhifadhi mabaki ya miili kwa usalama zaidi kwa kuzingatia kanuni na taratibu za afya katika zoezi la uhamishaji wa miili, " Bi Eduardina Maganga.

Mkazi wa Kijiji cha Bunonga Mzee Mayila ameishukuru TRC kwa kuandaa zoezi kiuadilifu pamoja na Serikali ya Kijiji kwa kutoa eneo la kuhifadhia wapendwa wao.



Mwenyekiti wa kijiji cha Didia Bwana Zuberi Juma akizungumza na wananchi wa Didia waliotwaliwa ardhi kupisha mradi wa SGR kabla ya kuanza zoezi la kuhamisha makaburi, mkoani Shinyanga, Septemba 2022